


# TAMKO LA KIIMANI JUU YA KANUNI ZA VIWANDA VYA UCHENJUAJI



**Kundi la utenda kazi la viwanda vya uchenjuaji, vina makao yake Ji-jini Washington, D.C Marekan, lenye misingi ya Imani, haki za binadamu na mashirika ya mazingira vikihusika na madhara mabaya yatokanayo na viwanda hivi vya uchenjuaji kwa binadamu na ulim-wengu alisia.**

• • • • • • • • •

**Tukiwa ni watu wa Imani, tukifanya kazi kutokea Marekani na nje ya Marekani, tunashuhudia na kuziwezesha jamii mbalimbali zilizodhurika na makosa ya shughuli za uchenjuaji, kama vile shughuli za viwanda vya mafuta, migodi na ukataji wa magogo.** Tumeona kwamba mapokeo mabaya na miradi inayoongozwa visivyo, huweza kuleta migogoro, uharibifu wa afya za binadamu, uhamishaji watu kutoka kwenye kaya zao, kutoka kwenye ardhi zao za asili, uharibifu wa mazingira na rushwa. Uchunguzi wa madini wa viwanda vya uchenjuaji vinadhoofisha uchumi wa jamii, vimezuia maendeleo na vinakiuka haki za binadamu, katika Amerika, lakini zaidi hasa katika Latin Amerika na bara la Asia (Hindi).

**Taratibu zetu zenye mchanganyiko wa imani, hutufanya tuheshimu na kulinda uumbaji wa Mwenyezi Mungu, kusimama kidete pamoja na jamii na wafanya kazi ambao huweza kuhamishwa, na kupoteza mali zao na matishio ya kiusalamu wao. Jitihada hizi zinahakikisha uhakika katika hali hizo, lakini hasa katika ulinzi wa jamii zenye mazingira magumu.**

Baadhi ya mashirika ya uchenjuaji zimekuwa na sera za ushirikishaji wa jamii au kujali zaidi utendaji ambao utakuwa utafanya madhara kidogo. Baadhi ya makampuni yamejiunga na kutekeleza ilani zenye kukubalika ilani hii, kama mashikika yafuatayo:- ‘THE UNITED NATIONS GLOBAL COMPACT’; ‘EXTRACTIVE INDUSTRIES TRANSPARENCY INITIATIVE (EITI)’; ‘GLOBAL REPORTING INITIATIVE AND VOLUNTARY PRINCIPLES ON SECURITY AND HUMAN RIGHTS’.

**Hata hivyo tunahitaji kufanya zaidi ya hayo. Serikali zote, mashirika na Taasisi za fedha ni lazima zishirikishe jamii zilizodhurika vikihusisha, viongozi wa mashirika za kiimani na kijamii hadi kufikia makubaliano ya pamoja kati ya vyama vyote.**

Serikali, mashirika ya fedha ya kimataifa na mashirika ya uchumi lazima yazingatie misingi ya uwazi na uhusishaji wa jamii na serikali. Lazima ziwe na mbinu za ulinzi wa jamii kutokana na uharibifu unaotikana na miradi hii katika mazingira, kifedha na kisheria.

Tuna nia ya kupunguza matumizi mabaya ya mazingira ya uumbaji wa Mwenyezi Mungu, lakini utendaji huu unapotokea utajiri wa mali asili unatakiwa utumike kuboresha maisha ya jamii inayozunguka miradi hiyo.

Tunazitaka serikali mbalimbali, taasisi za fedha ya kimataifa na mashirika kusimama imara na kujikita katika kanuni ambazo zitatoa mahusiano kwa wafanya kazi, raia wa kawaida na jamii vile vile kuhakikisha kuwa, mazingira, maisha ya binadamu na haki zao vinaheshimika!

Contact:  
Susan Thompson  
Medical Mission Sisters  
Alliance for Justice  
[susanstarrthompson@juno.com](mailto:susanstarrthompson@juno.com)

# **Tunashauri wale wanaohusika na viwanda hivi vy a uchenjuaji wazingatie kanuni zifuatazo:-**

1. Jamii husika ina haki ya kushirikishwa na kusikilizwa katika uchunguzi wa mali asili na uendelezaji wa eneo lao. Kwa hiyo, viwanda vya uchenjuaji ni lazima vizingatie sera zinazoelekeza upatikanaji wa ushirikishwaji wa jamii husika kwa mapana na utayari – (**Ushirikishwaji huru na kabla (Free Prior and Informed consent – FPIC.)**) kabla ya kuanza shughuli za kimradi. Ushirikishwaji huu uiwezesha jamii kuwa na haki ya kuukataa mradi huo.
2. Sera na maamuzi kuhusu viwanda hivi, ziwe za wazi bila kificho na zihusishe ushirikishwaji wenye maana wa wadau.
3. Viwanda hivi ni lazima vizingatie manufaa ya pande zote na kutathmini madhara katika mazingira hasa wahanga zaidi kama wanawake, wenyeji wa sehemu husika ambao ni watu fukara.
4. Viwanda ni lazima viajiri wafanya kazi kutoka jamii husika na visaidie kutoa fedha katika miradi ya kijamii, elimu, miradi ya maendeleo ili kukuza jamii na taifa kiuchumi na kuhakikisha ukuaji unaoridhisha.
5. Viwanda ni lazima viheshimu vyombo vya serikali za nchi kwa kushirikiana na jamii ya wafanya kazi, pamoja na mashirika yasiyo ya serekali, wakifanya kazi kwa pamoja na kuweka sera husika kwa maendeleo na ustawi wa jamii na outo wa asili.
6. Ili kuhakikisha haki inatendeka kwa familia zilizodhurika na jamii; mtu wa tatu ni lazima ashirikishwe katika utatuzi wa migogoro.
7. Ili kutekeleza azimio la Umoja wa Mataifa juu ya Haki za Binadamu, viwanda hivi vya uchenjuaji ni lazima viheshimu na kusaidia kulinda heshima ya binadamu pamoja na ulinzi wa vyanzo vinyavyotumika kwa pamoja na jamii hiyo na uendelezaji wa mali asili.
8. Viwanda vya uchenjuaji lazima viheshimu haki za upinzani toka kwa jamii au mashirika yanayoonesha upinzani, kupitia mandamano , mazungumzo na njia zingine zisizo na uhasama.

## **Waweka saini:-**

Africa Faith and Justice Network  
American Jewish World Service  
Caretakers of God's Creation of the United Methodist Church  
Columban Center for Advocacy and Outreach  
Conference of Major Superiors of Men (CMSM)  
JPIC Committee; Divine Word Missionaries, Chicago Province  
Franciscan Action Network  
Loretto Earth Network

Missionary Oblates of Mary Immaculate Justice, Peace, & Integrity of Creation Office  
Maryknoll Office for Global Concerns  
Medical Mission Sisters Alliance for Justice  
Sisters of Notre Dame de Namur Justice & Peace, Integrity of Creation Office  
Sisters of Mercy of the Americas Institute Justice Team  
The U.S. Jesuit Conference